## FUNZO LA 39

1. Je, kiongozi mpya aliyechaguliwa na Mungu badala ya Musa ni nani?
-Yoshua.

2. Je, Mungu alitimiza ahadi yake na kuwapa uzao wa Ibrahamu nchi ya Kanaani?
-Ndiyo.

3. Baada ya Yoshua kufa, Waisraeli walifanya nini?
-Baada ya Yoshua kufa, Waisraeli walimkataa Mungu na wakawa waovu sana.
-Baada ya Yoshua kufa, Waisraeli walijifanyia mifano na kuiabudu badala ya Mungu.

4. Je, ni nani aliyewadanganya Waisraeli hadi wakamkataa Mungu na kuabudu mifano?
-Shetani.

5. Je, tunapoabudu kitu kingine isipokuwa Mungu, tunamwabudu nani?
-Shetani.

6. Je, kwa nini Shetani anawaongoza watu kuabudu mifano?
-Kwa sababu Shetani anamchukia Mungu na hataki mtu yeyote amwabudu Mungu.
-Kwa sababu Shetani anawachukia watu wote na hataki mtu yeyote aokolewe na Mungu.



7. Je, Mungu aliwaadhibu vipi Waisraeli kwa kuabudu mifano?
-Mungu aliwatuma adui wa Israeli kuharibu mimea ya Waisraeli.
-Mungu aliwatuma adui wa Israeli kuja na kuwaibia mifugo yao yote.
-Mungu aliwatuma adui wa Israeli kuja na kuwafanya Waisraeli watumwa wao.

8. Je, Waisraeli walipotubu dhambi zao na kumwomba Mungu awasaidie, Mungu alifanya nini?
-Israeli walipotubu dhambi zao na kumwomba Mungu awasaidie, Mungu aliwachagua wanaume na wanawake ambao aliwatumia kuwaongoza Waisraeli kuwashinda adui zao.

9. Je, hao wanaume na wanawake ambao Mungu aliwachagua kuwaongoza Waisraeli kuwashinda adui zao waliitwaje?
-Waamuzi.

10. Je, kwa nini Mungu aliwapenda na kuwalinda Waisraeli?
-Kwa sababu Mungu aliahidi Ibrahamu, Isaka na Yakobo kuwa uzao wao utakuwa mwingi na utakuwa taifa kubwa.
-Kwa sababu Mungu aliahidi kumtuma Mwokozi kupitia kwa uzao wa Waisraeli.
-Kwa sababu Mungu aliahidi kutuma ujumbe wake, Biblia, kupitia kwa uzao wa Waisraeli.

11. Je, muamuzi wa mwisho wa Iraeli alikuwa nani?
-Samueli.

12. Kabla ya Samueli kufa, Waisraeli walimwambia afanye nini?
-Waisraeli walimwomba Samueli awachagulie mfalme awaongoze.

13. Je, kwa nini hii ilimhuzunisha Samueli?
-Samueli alihuzunika kwa sababu Israeli ilimkataa Mungu kuwa mfalme wao.

-Mungu alimchagua Sauli awe mfalme wa kwanza wa Israeli.

-Kwa sababu Mungu alimchagua Sauli alimtaka Sauli amtii lakini Sauli hakumtii Mungu.

-Hivyo basi, Samueli alimwambia Sauli kuwa Mungu alimchangua mtu mwingine awe mfalme.

Tusome 1 Samueli 13:13-14

13-Naye Samweli akamwambia Sauli, Umefanya upumbavu; hukuishika amri ya Bwana, Mungu wako, aliyokuamuru; kwa maana Bwana angaliufanya ufalme wako kuwa imara juu ya Israeli milele.
14-Lakini sasa ufalme wako hautadumu; Bwana amejitafutia mtu aupendezaye moyo wake, naye Bwana amemwamuru yeye kuwa mkuu juu ya watu wake, kwa sababu wewe hukulishika neno lile Bwana alilokuamuru.

-Je, Sauli alipokataa kumtii Mungu, Mungu alimchagua nani awe mfalme wa pili?



-Daudi.

-Mungu alimchagua Daudi awe mfalme wa pili wa Israeli.

Tusome 1 Samueli 16:1 & 13

1-Bwana akamwambia Samweli, Hata lini utamlilia Sauli, ikiwa mimi nimemkataa asiwamiliki Israeli? Ijaze pembe yako mafuta, uende, nami nitakupeleka kwa Yese, Mbethlehemi; maana nimejipatia mfalme katika wanawe.
13-Ndipo Samweli akaitwaa pembe yenye mafuta, akamtia mafuta kati ya ndugu zake; na roho ya Bwana ikamjilia Daudi kwa nguvu tangu siku ile. Basi Samweli akaondoka, akaenda zake Rama.

-Baada ya Sauli kufa, Waisraeli wote walimwendea Daudi na kumfanya kuwa mfalme wa Israeli.

Tusome 2 Samueli 5:1-4

1-Ndipo kabila zote za Israeli wakamwendea Daudi huko Hebroni, wakasema naye, wakinena, Tazama, sisi tu mfupa wako na nyama yako.
2-Zamani za kale, hapo Sauli alipokuwa mfalme juu yetu, wewe ndiwe uliyewaongoza Israeli watoke nje, na kuingia ndani. Naye Bwana akakuambia, Wewe utawalisha watu wangu Israeli, nawe utakuwa mkuu juu ya Israeli.
3-Basi wazee wote wa Israeli wakamwendea mfalme huko Hebroni, naye mfalme Daudi akapatana nao huko Hebroni mbele za Bwana; wakamtia Daudi mafuta awe mfalme juu ya

Israeli.
4-Daudi alikuwa amepata miaka thelathini alipoanza kutawala, akatawala miaka arobaini.

-Je, tofauti kati ya Daudi na Sauli ilikuwa gani?

-Sauli hakuamini kuwa alizaliwa katika dhambi na kutengana na Mungu.

-Lakini Daudi alijua kuwa alizaliwa katika dhambi na kutengana na Mungu.

-Sauli hakuamini kuwa Mungu huadhibu dhambi yote kwa kifo.

-Lakini Daudi alijua kuwa Mungu huadhibu dhambi yote kwa kifo.

-Sauli hakuamini kuwa ni Mungu pekee aliyeweza kumuokoa.

-Lakini Daudi alijua kuwa ni Mungu pekee aliyeweza kumuokoa.

-Sauli hakuamini ahadi ya Mungu ya kumtuma Mwokozi.

-Lakini Daudi aliamini kuwa Mungu atamtuma Mwokozi amuokoe kutoka kwa Shetani na kifo.

-Kwa sababu Daudi alimwamini Mungu, aliandika nyimbo nyingi za kumuabudu Mungu.



-Daudi aliandika nyimbo nyingi za kumuabudu Mungu ambazo sasa ziko katika Kitabu cha Mungu, Biblia.

-Kwa sababu Daudi alikuwa mfalme wa Israeli, alikuwa na pesa nyingi.

- Kwa sababu Daudi alikuwa mfalme wa Israeli, alijenga nyumba kubwa ya mbao, mawe, dhahabu na fedha.

-Siku moja, Daudi alianza kufikiri kuhusu nyumba yake na hema ya Mungu.

Tusome 2 Samueli 7:1-3

1-Ikawa, mfalme alipokuwa akikaa katika nyumba yake, hapo Bwana alipomstarehesha, asiudhiwe na adui zake waliomzunguka pande zote,
2-mfalme akamwambia Nathani, nabii, Angalia sasa, mimi ninakaa katika nyumba ya mierezi, bali sanduku la Mungu linakaa ndani ya mapazia.
3-Nathani akamwambia mfalme, Haya, fanya yote yaliyomo moyoni mwako; maana Bwana yu pamoja nawe.

-Je, baada ya Daudi kumaliza kujenga nyumba yake, alitaka kufanya nini?

-Daudi alitaka kumjengea Mungu nyumba.

-Je, Mungu anaitaji nyumba ya kuishi?
-La.

-Mungu yuko kila mahali wakati wowote na haitaji nyumba ya kuishi.

-Ingawaje Mungu haitaji nyumba ya kuishi, alifurahishwa na jinsi Daudi alivyomuwazia.

-Je, Mungu alimwambia nini Daudi?

Tusome 2 Samueli 7:12-13a

12-Nawe siku zako zitakapotimia, ukalala na baba zako, nitainua mzao wako nyuma yako, atakayetoka viunoni mwako, nami nitaufanya imara ufalme wake.
13-Yeye ndiye atakayejenga nyumba kwa jina langu,

-Ingawaje Mungu alifurahi kuwa Daudi alimuwaza, alimwambia Daudi kuwa si yeye atakae mjengea nyumba.

-Je, ni nani aliyestahili kumjengea Mungu nyumba?
-Mwana wa Daudi, Suleimani.

-Kwa sababu Daudi alimwamini Mungu, Mungu alimpa Daudi ahadi.

-Ifuatayo ni ahadi ambayo Mungu alimpa Daudi:

Tusome 2 Samueli 7:16

16-Na nyumba yako, na ufalme wako, vitathibitishwa milele mbele yako. Nacho kiti chako kitafanywa imara milele.



-Je, ahadi kubwa ambayo Mungu alimuahidi Daudi ilikuwa gani?

-Mungu alimuahidi kuwa atatuma Mwokozi kupitia uzao wa Daudi.

-Hii ahadi ambayo Mungu alimpa Daudi, ndiyo ile ambayo Mungu aliwapa Ibrahamu, Isaka na Yakobo.

-Mungu atamtuma Mwokozi ambaye atakuwa mfalme milele na milele.

-Je, Mungu alisahau ahadi yake ya kumtuma Mwokozi?
-La.

-Mungu wakati wote alikumbuka ahadi yake ya kumtuma Mwokozi kutuokoa kutoka kwa dhambi, Shetani na kifo.

-Kabla ya Daudi kufa, alifanya maandalizi mengi ya kumjengea Mungu nyumba.

-Kisha, Daudi alimpa Sulemani, mwanawe, kazi ya kujenga nyumba ya Mungu.

Tusome 1 Mambo ya Nyakati 22:5-6

5-Daudi akasema, Sulemani mwanangu akali ni mchanga bado, na mwororo, nayo nyumba atakayojengewa Bwana haina budi kuwa nzuri mno, yenye sifa na yenye fahari katika nchi zote; kwa hiyo mimi nitaiwekea akiba. Basi Daudi akaweka

akiba tele kabla hajafa.

6-Ndipo akamwita Sulemani mwanawe, akamwagiza amjengee Bwana, Mungu wa Israeli, nyumba.

-Kabla ya Daudi kufa, alimwambia mwanawe Sulemani amjengee Mungu nyumba.

-Baadaye, Daudi akafa, na Sulemani mwanawe akawa mfalme.

Tusome 1 Mambo ya Nyakati 29:26-28

26-Basi Daudi, mwana wa Yese, akawa mfalme juu ya Israeli wote.

27-Na wakati aliotawala juu ya Israeli, ulikuwa miaka arobaini; miaka saba alitawala Hebroni, na miaka thelathini na mitatu akatawala Yerusalemu.

28-Akafa mwenye umri mwema, ameshiba siku, na mali, na heshima; naye Sulemani mwanawe akamiliki badala yake.

-Baada ya Sulemani kuwa mfalme wa Israeli, alifanya nini?

Tusome 2 Mambo ya Nyakati 2:1a

1-Basi Sulemani alikusudia kujenga nyumba kwa jina la Bwana,

-Kama vile baba yake Daudi alivyomuagiza, Sulemani alimjengea Mungu nyumba.



-Jina ya nyumba ambayo Sulemani alimjengea Mungu iliitwa Hekalu.

-Sulemani alijenga hekalu katika mji wa Yerusalemu.

-Mji wa Yerusalemu ulikuwa mji mkubwa katika nchi ya Kanaani walipoishi Waisraeli.

-Ukuta mkubwa wa mawe ulizingira huo mji ili kuwalinda Waisraeli kutokana na adui zake.

-Hekalu aliyomjengea Mungu Sulemani ilikuwa kama hema ambayo Waisraeli walimjengea Mungu jangwani.

-Je, hekalu aliyomjengea Mungu Sulemani ilifananaje na hema ambayo Waisraeli walimjengea Mungu jangwani?

-Hema ya Mungu ilikuwa na chumba cha kwanza kilichoitwa Chumba Kitakatifu.

-Hekalu pia ilikuwa na chumba cha kwanza kilichoitwa Chumba Kitakatifu.

-Hema ya Mungu ilikuwa na chumba cha pili kilichoitwa Chumba Kitakatifu Zaidi.

-Hekalu pia ilikuwa na chumba cha pili kilichoitwa Chumba Kitakatifu Zaidi.

-Hema ya Mungu ilikuwa na pazia ambayo ilitenganisha hivyo vyumba viwili.

-Hekalu pia ilikuwa na pazia iliyotenganisha hivyo vyumba viwili.

-Je, kwa sababu Mungu ni mtakatifu na anachukia dhambi yote, ni mara ngapi kuhani mkuu aliruhusiwa kuingia katika Chumba Kitakatifu Zaidi?

-Mara moja kwa mwaka.

-Je, kwa sababu Mungu ni mtakatifu na anachukia dhambi yote, kuhani mkuu alifanya nini katika Chumba Kitakatifu Zaidi?

-Alinyunyuza damu ya mnyama juu ya Sanduku la Agano.

-Je, Mungu alifanya nini alipoona damu aliyonyunyuza kuhani mkuu juu ya Sanduku la Agano?

-Mungu alizuia adhabu ya dhambi kwa watu kwa mwaka mmoja hadi siku ambayo malipo bora ya dhambi yatakapofanywa.

-Je, damu ya mnyama iliweza kulipia dhambi za watu?
-La.

-Je, ni kwa nini damu ya mnyama haikuweza kulipia dhambi za watu?



-Kwa sababu dhambi lazima ilipwe kwa kifo cha mwenye dhambi.

-Baada ya Sulemani kufa, nini kilichowafanyikia Waisraeli?

-Waisraeli hawakukubaliana nani awe mfalme anayefuata.

-Hivyo basi makabila kumi na mbili ya Israeli yaligawanyika wakawa makundi mawili.

-Makabila kumi ya kaskazini yalitengana na makabila mawili ya kusini.

-Je, makabila kumi ya kaskazini yaliitwaje?
-Israeli.

-Je, makabila mawili ya kusini yaliitwaje?
-Yuda.

-Wafalme wengi walitawala Israeli na wafalme wengi walitawala Yuda.

-Wengi wa hao wafalme hawakumwamini Mungu.

-Ni wachache kati yao waliomwamini Mungu.